JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## KUSITISHWA KWA MUDA LESENI ZA HUDUMA ZA MAUDHUI MTANDAONI ZILIZOTOLEWA KWA MWANANCHI COMMUNICATIONS LIMITED

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania, Sheria Na. 12 ya mwaka 2003, kusimamia huduma za mawasiliano ya Kielektroniki na Posta katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa nyakati tofauti kati ya mwaka 2023 na 2024, TCRA ilitoa leseni za huduma za maudhui mtandaoni (online media services licences) kwa kampuni ya Mwananchi Communications Limited kutoa huduma kwa majina ya *The Citizen*, *Mwananchi Digital*, *Mwananchi* na *Mwanaspoti* kwa ajili ya utoaji wa huduma za maudhui mtandaoni nchini. Katika utoaji wa huduma na kwa mujibu wa Kanuni ya 16 ya Kanuni za Maudhui Mtandao (the Online Content Regulations) za mwaka 2020, Mwananchi Communications Limited anatakiwa kutokutangaza au kuchapisha kwa Umma maudhui yaliyozuiwa ikiwa ni pamoja na maudhui yanayolenga kudhihaki au kuharibu taswira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tarehe 01 Oktoba 2024 Mwananchi Communications Limited ilichapisha maudhui mjongeo na sauti (audio-visual content) kwenye mitandao yake ya kijamii, maudhui yaliyozuiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 16 ya Kanuni za Maudhui Mtandaoni zilizorejewa hapo juu. Aidha, maudhui hayo yameleta tafsiri hasi kwa Taifa, jambo ambalo linaathiri na kuharibu umoja, amani na mshikamano wa kitaifa.

**UMMA UNATAARIFIWA KUWA,** kufuatia kuchapishwa kwa maudhui yaliyokatazwa na yanayopingana na sheria, TCRA imesitisha kwa muda leseni za huduma za maudhui mtandaoni (online media services licences) za Mwananchi Communications Limited *(The Citizen, Mwananchi Digital, Mwananchi na Mwanaspoti)* kutoa huduma za maudhui mtandaoni nchini Tanzania kwa muda wa siku thelathini (30) tangu tarehe ya kutolewa kwa taarifa hii, wakati masuala mengine ya kiusimamizi yanafanyiwa kazi.

Imetolewa tarehe **02 Oktoba, 2024**

Dkt. Jabiri K. Bakari

**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz